MAOMBI A CHAGAMBA

JINSI YA KUSOMA RIPOTI ZA FEDHA

YALIYOMO

SURA YA KWANZA 6
JINSI YA KUSOMA RIPOTI YA HALI YA FEDHA (BALANCE SHEET) 6
SURA YA PILI 20
NAMNA YA KUSOMA RIPOTI YA MAPATO NA MATUMIZI 20
SURA YA TATU 30
JINSI YA KUSOMA RIPOTI YA MTIRIRIKO WA FEDHA (CASHFLOW) 30
SURA YA NNE 35
JINSI YA KUTUMIA RIPOTI YA FEDHA KUONGEZA UFANISI KATIKA MSHAHARA 35
SURA YA TANO 55
JINSI YA KUTUMIA RIPOTI YA FEDHA KUONGEZA FAIDA KATIKA BIASHARA 55
HITIMISHO 62

SURA YA NNE

JINSI YA KUTUMIA RIPOTI YA FEDHA KUONGEZA UFANISI KATIKA MSHAHARA

Sehemu ya pili ni namna ambavyo ripoti ya fedha inavyoweza kuongeza ufanisi wa matumizi ya mshahara.

Sasa kama sehemu ya kwanza haukuelewa basi naomba hii sehemu ya pili tuwe pamoja ili uweze kujifunza na hata kubadili hali yako ya maisha ya kifedha

Stori ya mwajiri na mfanyakazi wake

Kulikuwa na mmiliki wa kampuni moja (jina kapuni) alikuwa na meneja ambaye alikuwa ni kijana wa miaka 36 hivi, huyu kijana alikuwa meneja wa kampuni ya huyu mzee na kwa hali ya kitanzania alionekana kama ni kijana mwenye mafanikio kwani alikuwa na gari ya kutembelea na nyumba ya kuishi na familia nzuri ila alikuwa na changamoto ya kifedha karibuni kila mwezi, sasa kwa kuwa yeye na mwajiri wake walikuwa karibu, na huyu mwajiri alikuwa na miaka kama 50 hivi, kwa hiyo utaona walikuwa kama mtu na mdogo wake, akaamua kumuona bosi wake kwa ushauri wa tatizo lake la fedha, mazungumzo yao yalikuwa hivi.

***Kijana*:** bosi mimi nina changamoto ya kifedha, ijapokuwa nafanya kazi na ninaingiza pesa ila changamoto ya kipesa bado ipo, yaani mshahara mmoja haukutani na mshahara mwingine, kuna kitu ambacho unaweza kunisaidia?

***Bosi*:** huku akicheka, akamwambia kijana, ndio ninaweza kukusaidia ila sina uhakika kama uko tayari kulipa gharama ya kitu ambacho nitakufundisha.

***Kijana*:** bosi mimi niko tayari kulipa gharama yoyote ile, ili nijifunze kuwa na uhuru wa kifedha.

***Bosi*:** kweli? (Bosi aliuliza kwa mkazo).

Kijana : huku akiapa, MUNGU mmoja chochote kile utakacho niambia nitafanya.

***Bosi*:** akamwambia kijana, andika hapa (huku akimsogezea karatasi) sema chochote kile ambacho bosi atakifanya ili kunifundisha mimi nitakubaliana nacho,na weka sahihi yako hapa.

***Kijana*:** akaweka sahihi yake haraka sana

***Bosi*:** akamwambia kijana, naomba uniletee waraka wako wewe wa hali ya fedha (the balace sheet) wa mwezi uliopita.

***Kijana*:** akapigwa na butwaa, kwani toka aanze kufanya kazi kama meneja hajawahi kusikia kuna waraka wa hali ya fedha (balance sheet ya mtu binafsi), ila kwa kuwa ameshasaini kuwa chochote atafanya ili kujifunza, akaondoka na kwenda kuuliza kwa marafiki zake anawezaje kuandaa waraka wa hali ya fedha akapata majibu akaanza kazi.

Kabla hatujaendelea na somo letu la bosi na meneja wake, tujikumbushe kitu ambacho tumesoma katika sehemu ya kwanza kuhusu waraka wa hali ya fedha (balance sheet).

Katika kipengele kilichopita tumeona ya kuwa waraka huu una pande mbili, upande wa kwanza ni upande wa mtaji (pesa za wanahisa pamoja na madeni) tukasema huu mtaji ndio unaotumika kununua mali ambazo kampuni inakuwa nazo, kwa hiyo ukiona magari au mitambo na mali nyingine ambazo kampuni inakuwa nazo basi ujue vimenunuliwa kwa pesa zilizopo katika upande wa mtaji.

Waraka wa hali ya fedha ni kama picha ambayo inapigwa kwa kipindi fulani kuonyesha hali ya kampuni au mtu binafsi, yaani inakuwa hivi tunakuja kwako tunapiga picha ya kila kitu ulichonacho na baada ya hapo tuna thaminisha kila kitu na tunaandika waraka wa hali yako ya kifedha.

Nikupe mfano kama tukitaka kuandika waraka wa hali ya kedha wa kwako hapo hapo ulipo (*namaanisha sasa hivi unaposoma hiki kitabu)* basi unaweza kuwa na pesa mfukoni, simu au kompyuta unayotumia kusomea, nguo ulizovaa na viatu, kwa hiyo kama tuna kutengenezea waraka wako wa fedha utakuwa hivi.

Waraka wa hali ya fedha

Waraka wa hali ya fedha (balance sheet)	**Pesa katika maelfu**
laptop	700000/=
Simu	500000/=
Nguo na viatu	70000/=
Jumla kuu	**1270000/=**
Pesa za wamiliki na madeni	**Pesa katika maelfu**
Pesa za wamiliki	570000/=
Madeni	700000/=
Jumla kuu	**1270000/=**

Kwa hiyo tunaweza kusema waraka wako wa hali ya fedha una thamani ya 1270000/= ila katika pesa ulizotumia kununua mali hizi, 570000/= ni pesa yako mwenyewe na 700000/= ni pesa ambayo umekopa, nadhani kama tulikuwa pamoja katika kipengele cha kwanza utakuwa umesha elewa na unajua nini hali ya huyu mtu.

Kama sikukosei na kijana wetu atatuletea mzigo unao fanana na huo ambao tumeuona.

Turudi katika mazungumzo yetu ya bosi na kijana wake

Baada ya wiki moja ya kuumiza kichwa *(kuchana mikeka na kila kitu)* kijana akaja na ripoti yake ya hali ya fedha ambayo ilikuwa hivi.

Ripoti ya hali ya fedha ya mwezi wa kwanza

Mali	Pesa katika mamilioni
Mali za muda mrefu	
Nyumba ya kuishi	150
Gari la kutembelea la kijana	30
Gari la kutembelea la mke wake	15
Mali za kielectronic (kompyuta,tv,friji nk	10
Vitu vingine vya nyumbani	15
Mali za muda mfupi	
Pesa benki	2
Jumla	**222**
Madeni na pesa za mmiliki	
Madeni ya muda mrefu	Pesa katika mamilioni
Mkopo wa nyumba	80
Mkopo wa gari	5
Madeni ya muda mfupi	
Riba ya nyumba	1
Riba ya gari	0.375
Bili za umeme na maji	0.1
Jumla	**86.475**
Pesa za mmiliki	135.525

Duuh! Mi niko vizuri kwenye kuotea (*kubahatisha*), kijana wetu amekuja na mzigo kama ule ambao nimetabiri (*inabidi nianze ku bet, kumbe niko vizuri)*.

Kwa hali ya kitanzania huyu jamaa ana maisha mazuri kwani ukiondoa madeni aliyonayo anabakiwa na mali zake mwenyewe zenye thamani ya milioni 135.525, kifupi kijana ni milionea tayari. *(kwa ripoti nzuri namna hii kwa kijana wa miaka 36 mimi ngoja nitabiri tena kuwa bosi wake atamfukuza kazi akidhani kijana anamuibia hela).*

Sasa baada ya kuandaa hii ripoti akaiwasilisha kwa bosi wake, bosi wake akaiangalia tu sekunde chache akacheka *(ujue ukijua jinsi ya kusoma ripoti ya fedha, unakua sawa sawa na daktari bingwa wa masuala ya fedha),* ujue msema kweli wa hali ya mtu ya kifedha sio anavyoonekana bali waraka wake wa kifedha ndio unasema kila kitu.

Bosi akamwambia kijana, sawa nimeona ripoti yako nitakujulisha nikiwa tayari, *(haa! Jamaa hajamfukuza dogo kazi?, hapo ningekuwa nime bet mkeka ungekuwa umechanika)* baada ya hapo wakaagana. Ilipofika mwisho wa mwezi kijana anaenda benki akakuta mshahara hakuna, akatoka amepaniki akaenda moja kwa moja mpaka ofisini kumuona muhasibu, akauliza kwa hasira *kwa nini haujaweka mshahara wangu mwezi huu?* Muhasibu akajibu bosi amesema ukija nikupe hii notisi, akamuonyesha ile notisi ambayo jamaa ali saini mwezi uliopita akiomba kufundishwa.

Jamaa akatoka pale ofisini akiwa mdogo kama pilitoni (amedhoofu), na mawazo kibao kichwani, ikaenda mpaka mwezi ukaisha (*wakati huo jamaa alikuwa hataki*

hata kumuangalia bosi wake, kijana kichwani mwake alikuwa anawaza, huku kufundishana gani tunanyimana mshahara, asiponipa mshahara mwezi huu naenda kuvunja mkataba wa kufundishana), mwezi huu kijana akapata mshahara wake kama kawaida.

Bosi akamwita kijana akasema naomba ripoti yako ya hali ya fedha mwezi huu, jamaa akaileta haraka sana na ilikuwa kama ifuatavyo.

Ripoti ya hali ya fedha ya mwezi wa pili

Mali	Pesa katika mamilioni
Mali za muda mrefu	
Nyumba ya kuishi	150
Gari la kutembelea la kijana	30
Mali za kielectronic (kompyuta,tv,friji nk	10
Vitu vingine vya nyumbani	15
Mali za muda mfupi	
Pesa benki	3
Jumla	208
Madeni na pesa za mmiliki	
Madeni ya muda mrefu	Pesa katika mamilioni
Mkopo wa nyumba	80
Mkopo wa gari	5
Madeni ya muda mfupi	
Riba ya nyumba	1
Riba ya gari	0.375
Bili za umeme na maji	0.1
Jumla	86.475
Pesa za mmiliki	121.525

Bosi wake alipo ona ripoti ya mwezi huu wa pili akacheka sana *(kijana hapa ana hasira za kutolipwa mshahara mwezi uliopita)* akasema kwa sauti kumbe gari ya mke wako ndio imepita kushoto (imeuzwa), kama umechunguza ripoti hii ina tofauti na ripoti iliyopita kwani utajiri wa kijana umepungua kutoka milioni 135.525 mpaka milioni 121.525, na kama umechunguza ni kuwa gari la mke wa kijana halipo tena kwenye waraka, hapo in maana limeuzwa na kama umechunguza pesa benki pia imeongezeka, kwani baada ya kuuza gari kuna hela ilibaki.

SOMO LIKAANZA

Somo likaanza, bosi akasema sababu ambayo imefanya nikunyime mshahara mwezi uliopita ni kuwa nilitaka nikikuonyeshe ya kuwa ijapokuwa wewe ni milionea kwenye mali zako ila wewe ni masikini tu kama masikini wengine,*(duuh! Bosi ana maneno magumu, yaani amemchapa dongo kavu kijana wake wa kazi,kijana hakufurahia alichokisikia ila kwa kuwa ni bosi wake na mwalimu wake ikabidi awe mpole tu),* bosi akaendelea kusema, kama nisingekupa mshahara mwezi huu, mwezi ujao ungekuja mali zimepungua tena, na kama nikifanya hivi kwa miezi 7 mfululizo utabakiwa hauna kitu, huoni kama hauna tofauti na masikini wengine?.

Bosi akasema hivi, kama kampuni yangu ingekuwa na hali ya kifedha kama yako leo hii ningekuwa nimeshakufukuza kazi zamani sana, kwa sababu ili kampuni yangu iendelee kuwepo lazima iwe na uwezo wa kutengeneza ripoti ya mapato na matumizi ila mali zako hazina uwezo wa kutengeneza ripoti ya mapato na matumizi.*(bro chagamba hapa bosi ana maanisha nini tupe maelezo kidogo)*

NAJUA UNATAMANI KUJUA KILICHOENDELEA SI NDIYO?

PATA NAKALA YA KITABU HIKI (kurasa 62) PAMOJA NA KITABU KINGINE KINACHOITWA FALSAFA YA UWEKEZAJI (kurasa 54) KWA TSH 5000/= (*utapata vitabu hivi viwili, ambavyo viko katika mfumo wa pdf*)

JINSI YA KUPATA VITABU HIVI

Wasiliana na mwandishi kwa namba kwa simu au whatsapp. 0713999595,